



Sheria Mpya ya Kutangaza Tumbaku kwa Wauzaji wote wa Rejareja

Kuanzia tarehe 22 Septemba 2010

Marufuku kuonyesha matangazo ya bidhaa za tumbaku na vinavyowezesha uvutaji kwenye sehemu za rejareja.

Kuanzia tarehe 22 Septemba 2010 maduka ya rejareja hapa Western Australia yatapigwa marufuku kuonyesha picha za bidhaa zitokanazo na tumbaku na vinavyowezesha uvutaji.

Nini maana ya kupiga marufuku kuonyesha picha?

Wauza tumbaku rejareja inabidi kuhakikisha bidhaa za tumbaku, ukijumuisha vifurushi kimoja kimoja na makatoni ukijumuisha na vinavyowezesha uvutaji haviwezi kuonekana na umma kutoka ndani au nje ya majengo.

Kuona bila kutegemea

Upigaji marufuku kuonyesha haitumiki kipindi bidhaa zitokanazo na tumbaku, ikijumuisha pakiti na viwezesha uvutaji, vitakapoonyeshwa kwa mteja kufuatia ombi lake, hii inajumuisha kipindi cha mauzo/kuuza.

Kipindi muuzaji wa rejareja anapojazia bidhaa zake zitokanazo na tumbaku kuna uwezekano usiozuilika wa mtu aliyekwenye jamii kuweza kuona bidhaa zitokanazo na tumbaku au vinavyowezesha uvutaji.

Ni sera ya Idara ya Afya kuruhusu uwezekano wa kuona bila kutegemea ambao unaweza kutokea kutokana mazingira halali yenyewe kufuata taratibu za kibashara (kama vile kuongeza kwenye makabati au kuhesabu bidhaa zilizopo mbele ya umma). Lakini, wauzaji wa rejareja inabidi wahakikishe kuwa milango na vingine vinavyoziba sehemu za kuhifadhi haziachwi wazi kwa makusudi baada ya kumaliza kuongeza bidhaa kwani hii inaweza kusababisha uchukuliwe hatua.

Bei za Tiketi na Ubao unaoonyesha Bei

Kama ilivyokesi hivi sasa, maeleo kuhusu upatikanaji au bei za bidhaa za tumbaku zinaweza kuendelea kutolewa kwenye bei za tiketi na ubao unaoonyesha bei.

Kampeni ya Kuelimisha

Ukijumuisha na ushauri na washika dau kutoka kwenye nyanja tofauti kuhusiana na kampeni za kuelimisha zitafanyika. Hiyo itajumuisha elimu na kusambaza maeleo kwa njia tofauti kama vile: matangazo ya redioni; radio na matangazo ya magazetini; machapisho na kupitia kwenye mtandao wa intaneti.



Matangazo ya aina gani yanayohusiana na vitu vinavyowezesha uvutaji vinavyojumuisha upigaji marufuku kuonyesha picha?

Aina ya vitu vinavyowezesha uvutaji vinavyojumuishwa kwenye upigwaji marufuku kuonyeshwa ni:

- karatasi za sigara
- kiko
- chombo cha kushikia sigara
- mashine za kukunjia
- hookahs na kiko cha maji kinachotumika kwa ajili ya uvutaji wa bidhaa za tumbaku
- chombo kingine chochote kinachoweza kusaidia uvutaji wa tumbaku.

Viberiti na vya kuwashia sigara sio vitu vya uwezeshaji kwa hiyo havijumuishwi kwenye tangazo la upigaji marufuko kuonyeshwa na vinaweza kuendelea kuwekwa kwenye maonyesho.

Jinsi gani sheria itakavyoteklezwa?

Idara ya Afya Western Australia inaweka msisitizo na kulenga kwenye kuhakikisha ufuatiliaji na ukaguzi kutambua utekelezaji wake, hasa baada ya kuitishwa sheria mpya. Ukaguzi pia unaweza kufanyika kutokana na matokeo ya malalamiko ya wanajumuia.

Idara ya Afya inatumia mikakati mbalimbali kuwapa na kuongeza moyo wa utekelezaji ikijumuisha kutoa ushauri, kuelimisha, kutoa maonyo, au kuwashtaki.

Mawasiliano:

Tobacco Control Branch	Anwani ya Posta:
Grace Vaughan House	Department of Health
227 Stubbs Terrace	PO Box 1335
SHENTON PARK WA 6008	WEST LEEDERVILLE WA 6901
Telephone: 1300 784 892	Internet: www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol
Fax: (08) 9382 0770	

Disclaimer:

The information contained in this factsheet has been produced as a guide only.

To view the full details in the relevant Tobacco Control legislation, visit www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol

